Maine Center for Disease Control and Prevention
An Office of the Department of Health and Human Services

Ushauri wa Jinsi ya Kutumia Hundi za WIC za Chakula cha Mtoto Mchanga--angalia picha ya hundi iliyo hapa chini:

1. Ni muhimu sana kwamba ununue mchanganyiko wa chakula unaofaa kwa mtoto wako mchanga. Hundi za WIC za chakula cha mtoto mchanga huwa na jina la chakula cha mtoto mchanga ambacho mtoto wako anahitaji. Vyakula vyote vya watoto wachanga si sawa. Hundi za chakula cha mtoto mchanga hujumuisha vifuatavyo:

② **Ukubwa wa chupa ya chakula cha mtoto mchanga huwa kwenye hundi.** Chakula cha mtoto mchanga unachonunua ni lazima kiwe cha ukubwa unaolingana na ule ulioorodheshwa kwenye hundi.

③ **Aina ya chakula cha mtoto mchanga iko kwenye hundi:**

- Ya Unga
- Mchanganyiko uliokolea
- Chakula Kilicho Tayari Kupewa Mtoto

Chakula cha mtoto mchanga unachonunua ni lazima kiwe cha aina sawa na ile iliyoorodheshwa kwenye hundi.

④ **Jina la chakula cha mtoto mchanga iko kwenye hundi.** Chakula cha mtoto mchanga unachonunua ni lazima kilingane na kile kilichoorodheshwa kwenye hundi.

⑤ **Nambari 5 za mwisho za msimbo pau wa "UPC" kwenye chupa ya chakula cha mtoto mchanga.** Nambari hizi ni lazima zilingane na nambari za chakula cha mtoto mchanga ambacho unamnunulia mtoto wako.

Ikiwa una maswali kuhusu hundi za chakula cha mtoto mchanga, tafadhali wasiliana na ofisi yako ya WIC.